

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA

Simu Na: +255(026) 2502170  
Nukushi: +255(026) 2502078  
Barua Pepe: [ras@singida.go.tz](mailto:ras@singida.go.tz)  
Tovuti: <http://www.singida.go.tz>  
*Unapojibu tafadhali taja:*



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida,  
Mtaa wa Bomani,  
S.L.P 05,  
**SINGIDA.**

Kumb. Na. GA.202/381/01/68

18 Septemba, 2024

Mkurugenzi wa Manispaa,  
Halmashauri ya Manispaa,  
**Singida**

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri za Wilaya,  
**Itigi, Iramba, Manyoni, Mkalama, Ikungi na Singida.**

**Yah: HUDUMA ZA KIBINGWA NA UHINGWA BOBEZI AWAMU YA PILI KATIKA HOSPITALI 184 ZA HALMASHAURI “MADAKTARI WA RAIS DR. SAMIA” KUANZIA TAREHE 23 - 29 SEPTEMBER, 2024.**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

2. Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, imeandaa zoezi tajwa katika Mkoa wa Singida.

3. Kwa kipindi cha tarehe 6 Mei hadi 28 Juni 2024, awamu ya kwanza ya huduma za kibingwa na ubingwa bobezi zilifanyika katika vituo vya kutolea huduma katika zoezi hilo wagonjwa 2725 walihudumiwa, watoa huduma 118 walijengewa uwezo katika fani mbalimbali na vile walifanikiwa kuimarisha utendaji wa “NICU” 5 zilizokuwepo na kuanzisha 23 katika vituo hivyo.

4. Kutokana na mafanikio makubwa ya awamu ya kwanza. Wizara ya Afya ikishirikiana na OR- TAMISEMI imepanga kufanya awamu ya pili ya zoezi hili itafanyika kuanzia tarehe **23 - 29 September, 2024** kwenye Hospitali 7 za ngazi ya Halmashauri kwa muda wa wiki moja. Kwa kila Hospitali itapokea seti ya madaktari bingwa sita na muuguzi bingwa mmoja ambao ni:-

- Daktari bingwa wa magonjwa ya wanawake na Ukunga (Obsetrician and Gynaecology).
- Daktari bingwa au bobesi wa watoto na watoto wachanga (Paediatrician/Neonatologist)
- Daktari Bingwa wa upasuaji au Mfumo wa mkojo (General surgeon/urologist)
- Daktari Bingwa wa usingizi na ganzi (Anaesthesiologist)
- Daktari Bingwa wa magonjwa ya ndani (Physician)
- Daktari Bingwa wa kinywa na Meno (Maxillofacial Surgeon)
- Muuguzi Bingwa na kila Halmashauri katika hospital moja ya Halmashauri iliyopo mjini itapata daktari mmoja wa mifupa na ajali (Orthopaedic and traumatology surgeon).

5. Kwa barua hii unaombwa kufanya manadalizi na uhamimashishaji wa kutosha ili shughuli hii iweze kufanyika kwa ufanisi unaostahili.

6. Nawatakia maandalizi mema.



Dkt. Fatuma R. Mganga  
**KATIBU TAWALA WA MKOA**

Nakala:- Makatibu Tawala wa Wilaya,  
**MKOA WA SINGIDA**